# TNMC Habari

Toleo N0. 010

TOLEO MAALUMU JULAI, 2024

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Waziri Mkuu Aongoza Maelfu Kushiriki NBC Marathon Jijini Dodoma.

Uk 01




- TNMC Yaunga Mkono Kwa kupelea Wakimbiaji 100

## Millioni 300

zakusanywa kusaidia mapambano dhidi ya Kansa ya Mlango wa shingo ya kizazi kwa wanawake

## TNMC yashiriki Maonesho ya Kitaifa ya Sabasaba




- Msajili aichambua Misingi Saba ya Kitaaluma.
- Vyombo vya Habari vya chambua Majukumu ya Baraza.

Uk 06

## Mtihani wa Usajili na Leseni kufanyika Agosti 23, 2024

Uk 02

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**

Bi. Agnes Mtawa

**MHARIRI**

Mwakapiso Ndimmyake

**WARATIBU**

Irene Chilewa
Rose Mhando

**MSANIFU JARIDA**

Ezekiel Nyalusi

P.O BOX1736 DODOMA
TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

# Waziri Mkuu Aongoza Maelfu Kushiriki NBC Marthon Jijini Dodoma




**Na Ezekiel Nyalusi**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, Mapema Julai 28, 2024 ameongoza mamia ya Wanariadha kwenye mbio za NBC Marathon zilizoandaliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC Bank) kwa lengo la kukusanya Fedha ili kusaidia matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi sanjari na elimu kwa Wakunga.

Mbio hizo za Kilomita 42, 21, 10, 5 ambazo Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC lilishiriki kwa kuwalipia ada ya ushiriki watumishi wake pamoja na wauguzi na wakunga waliyopo Mkoa wa Dodoma ambao jumla ya wauguzi na wakunga 90 walishiriki mbio hizo. lengo lilikuwa ni kuunga Mkono Marathoni hiyo ambayo lengo lake ni kuchangia matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake na ufadhili wa masomo kwa wauguzi na Wakunga. Mbio hizo zilianzia viwanja vya Jamhuri Mkoani Dodoma na kuishi katika viwanja hivyo.

Akihutubia maelfu ya washiriki mara baada ya kukamilika kwa mbio hizo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ameishukuru Benki ya Taifa ya Biashara NBC kuendelea kushirikiana na Serikali kuchangia na kuwezesha uboreshaji wa sekta ya Afya kwa maeneo yanayogusa Ustawi wa jamii.

**Millioni 300**

**zakusanywa kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya Mlango wa shingo ya kizazi kwa wanawake**

***"Mbio hizi zimekusanya michango mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Sekta ya Afya, NBC mmendelea kutuonyesha njia kwa ubunifu wenu wa kukusanya Fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye Sekta ya Afya, Fedha ambayo ameitaja Mkurugenzi Mkuu Millioni 300 ambayo itakabidhiwa leo ni kwa lengo ya kuusaidia mapambano dhidi ya saratani ya Mlango wa shingo ya kizazi kwa wanawake"***




NBC wamebainisha mgawavyo wa Fedha hizo, ambapo Shilingi Milioni 100 zitapelekwa Taasisi ya saratani ya Ocean Road, Millioni 100 kutumika kusomesha wauguzi na wakunga kupitia Taasisi Benjamini Mkapa na Milioni 50 kuchangia ujenzi wa Majengo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Baadhi ya Viongozi walioambatana na Waziri Mkuu ni pamoja na Naibu Waziri wa Michezo Sanaa na Utamaduni Mhe. Hamiss Mwinjuma, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt John Jingu, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Dkt. Mohamed Janabi, Mkurugenzi wa Huduma za kinga Ntuli Dkt. Kapologwe pamoja na mamia ya wananchi kutoka ndani na nje ya nchi.

# TNMC yashiriki Maonesho ya kimataifa ya Sabasaba

## ■ Msajili aichambua misingi saba ya kitaaluma




*Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa (wa kwanza kulia) akiwa katika Banda la TNMC katika Maonesho ya kitaifa ya Sabasaba Jijini Dar ES salaam.*

*Na Ezekiel Nyalusi*

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) limeshiriki maonesho ya kimataifa ya kibiashara yanayofanyika kila mwaka katika Jijini Dar es Salaam, ambapo mwaka huu yalianza Juni 28 na kuhitimishwa Julai 13. 2024

Katika Maonesho hayo watu zaidi ya 425 walifika kwenye banda la Baraza kwa ajili ya kujifunza na kulifahamu huku zaidi ya wauguzi na wakunga (200) walipata huduma za kuhuisha leseni, usajili wa awali (student Indexing) sambamba na huduma za elimu ya Maadili na sheria ya Uuguzi na Ukunga.

Katika maonesho hayo Msajili wa Baraza Bi. Agnes Mtawa, alipata wasaa kuelezea masuala mabalimbali ya Baraza ikiwa ni pamoja na misingi saba ya uuguzi na ukunga ambayo ni Kuthamini Utu na maisha ya Mtu, kabla ya kutoa huduma sharti Muuguzi na Mkunga apate ridhaa ya mpokea huduma kabla ya kutoa huduma, uwajibikaji wa kile unachokifanya, kufanya kazi kwa kushirikiana na wanataaluma wengine, kuwa mwaminifu na kutoa huduma bila upendeleo, Kutunza siri za Mteja na kujiendeleza kitaaluma.



Wananchi na wanataaluma waliofika kwenye Banda la TNMC walipongeza ushiriki wa Baraza kwenye maonesho haya kwa kuwa ilikuwa ni fursa muhimu kwao kulifahamu Baraza na kupatiwa huduma za papo kwa hapa.




***"Nimefurahi sana kufika hapa, leo nimejifunza kuhusu usajili wa awali Indexing, jambo hili tulikuwa hatulielewi vizuri sasa leo nimejua umuhimu wake na ni kwa mujibu wa Sheria hivyo nawahamasisha wanafunzii wenzagu wajisajili ili waweze tambulika na TMNC tangu wakiwa vyuoni"*** alisema Evidence Goldian, Rais wa Chama cha wanafunzi wa taaluma ya Uuguzi na Ukunga Chuo kikuu cha Muhimbili.

Maonesho hayo ya 48 yalifunguliwa na Rais wa Msumbini Mhe. Filipe Nyusi na kufungwa Julai 13, 2024 na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi.

# Mtihani wa usajili na Leseni Kufanyika Agosti 23, 2024



*Kutoka Maktaba; Watahiniwa wa Mtihani wa Usajili na Leseni Wakipata Maelezo ya taratibu za Mtihani siku moja kabla ya Mtihani*

***Na Mwandishi wetu***

Ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC inataraji kuratibu na kuendesha Mtihani wa usajili na leseni ambapo zaidi ya watahiniwa 3,000 wenye sifa wanatarajiwa kujisajili na kufanya Mtihani wa usaji na leseni, ambao humpa fursa Muuguzi au Mkunga kusajiliwa na kutoa huduma kama mwanataaluma baada ya kufaulu Mtihani huo.

Taarifa ya Msajili kwa umma, imebainisha sifa za watahiniwa wanaostahili kufanya Mtihani huo kuwa ni pamoja na kila mtahiniwa kuwa na namba ya utambulisho yaani (Indexing Number) kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha kanuni za mafunzo, kuweka picha sahihi (Passport Size 45X35), kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kufunzu elimu ya Sekondari pamoja na kufanya malipo kwa wakati na kuchagua kituo sahihi cha mtihani.

Aidha, taarifa hiyo imeendelea kutanabaisha kuwa Mtihani utafanyika Agosti 23,2024 katika vituo vinne (4) vilivyopo katika Mikoa mnne ambavyo ni chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) Jijini Dodoma, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) Jijini Mwanza, Taasisi ya Uhasibu Mbeya, Jijinini Mbeya na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) Jjijini Dar es Salaam.

Taarifa hiyo imesema kwamba, dirisha la maombi limefunguliwa na lipo wazi tangu tarehe 01/07/2024 na litafungwa mwezi huu tarehe 14/08/2024 na kuongeza kuwa Maombi yanatakiwa kufanyika kwa njia ya mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza *https://tnmcis.tnmc.go.tz/*

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) ni mamlaka ya Kisheria ikitekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga iliyotungwa na Bunge mwaka 2010, ambapo jukumu lake kuu ni kusimamia taaluma na wanataaluma wa kada ya Uuguzi na Ukunga ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wanataaluma hao ni salama kwa jamii lakini pia miongoni mwa majukumu yake mengine ni pamoja kuratibu na kuendesha Mtihani wa usajili na leseni.

# Msajili TNMC ashiriki Mahafali ya Kwanza ya Wahitimu wa Stashahada ya Uuguzi na Ukunga ST. Theresa



**Na Mwandishi wetu**

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga (TNMC)Tanzania Bi Agnes Mtawa, amewataka wauguzi na wakunga kuzingatia misingi saba ya taaluma yao wakati wote wanapotoa huduma kwa wagonjwa.

Msajili ametoa agizo hilo leo Julai 20, 2024 akiwa mgeni rasmi kwenye Mahafali ya kwanza ya Chuo cha Uuguzi na Ukunga cha St. Theresa, kilichopo Moshi Mkoniani Kilimanjaro.



***“Na katika taaluma hii tunamisingi saba ambayo ukiizingatia hii utabarikiwa na jamii yote na Mungu atakubariki, utashangaa baraza zitakuwa zinamiminika bila wewe kujua baraka hizi zinatoka wapi, lakini kumbe ni jinsi unavyohudumia wagonjwa”***

Ameitaja misingi hiyo kuwa ni pamoja na; Kuthamini utu na Maisha ya Mtu, lazima upate ridhaa ya mpokea huduma kabla hujatoa huduma, uwajibikaji wa kile unachokifanya, kufanya kazi kwa kushirikiana na wanataaluma wengine, kuwa mawaminifu na kutoa huduma bila upendeleo, Kutunza siri za Mteja sanjari na kujiendeleza kitaaluma.

Mahafali haya yalitanguliwa na misa maalumu ya shukrani katika kanisa la Mtakatifu Yohanne wa Pili lilipoko Soweto jimbo Katoliki la Moshi Mjini.



Akihubiri wakati akiongoza Misa hiyo maalumu ya shukrani kwa wahitimu hao, Mwashamu Baba Askofu Ludovick Minde, amesema kwa kuhitimu kwao katika taaluma hiyo, wanachukua nafasi ya juu sana katika jamii na ndio maana wanapewa mamlaka ya ajabu ya kuangalia mwili wa binadamu akiwa mtupu, kisha akawataka wakafanye kazi kwa upendo, upole na unyenyekevu.

***“Nendeni mkazidumishe fadhila za mtatifu Theresa katika utendaji kazi wenu, igeni maisha yake ya matendo mema, ninyi msipokuwa na matendo mema nani atatuudumia, mkimuacha Mungu, mkimuacha Yesu, hamuwezi kufanikiwa, wahitimu wetu tunamba sana mkastawi katika nyanja zote hasa hiyo ya upendo na kutabasamu kwa wagonjwa,makastawi sana”*** Alisisitiza Baba Askofu.

Jumla ya wahitimu 24 wametunukiwa vyeti katika Mahafali ya kwanza ya chuo hicho baada ya kuhitimu kwa ngazi ya stashahada katika taaluma za Uuguzi na Ukunga katika Mahafali iliyofanyika Mjini Moshi - Kilimanjaro.

# Wauguzi, wakunga Mkoani Shinyanga wanufaika na Nishati safi ya kupikia.



**Na Mwandishi Wetu**

Jumla ya wauguzi na wakunga 200 Mkoani Shinyanga wamenufaika na nishati safi ya kupikia ya gesi, iliyotolewa na Wadau wa Taasisi ya Doris Mollel, kisha wakaaswa kuendelea kutumia nishati hiyo salama badala ya kuni ambazo huzalisha moshi wenye madhara kiafya na mazingira

Rai hiyo imetolewa na Mbunge viti maalum Mkoa wa Shinyanga Mhe. Santiel Kirumba, Julai 09, 2024 wakati akikabidhi jumla ya mitungi 200 kwa watumishi wauguzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga, Hospitali ya Manispaa Shinyanga, Kituo cha Afya Kambarage, Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga na Kolandoto, iliyotolewa na wadau Doris Mollel Foundation pamoja na Kampuni ya uzalishaji gesi (Oryx Gas).




Mhe. Santiel, ameeleza matumizi ya kuni yamekuwa sababu kubwa ya uharibifu wa mazingira, lakini vilevile huhatarisha Afya haswa ya mama na Mtoto tumboni, sababu si salama, huku akisisitiza kuwepo kwa matumizi mazuri ya gesi ambayo itasaidia kulinda usalama wa Afya kwa Mama mjamzito.

***"Niwaombe wauguzi, mmekuwa mkipokea akina mama wengi katika maeneo yenu ya kazi ambao wanaelekea kujifungua, tutumie nishati safi ya kupikia ili kulinda maisha ya Mama na Mtoto, " tuachane kabisa na matumizi ya kuni ambayo huhatarisha Afya ya Mama mjamzito, licha ya hivyo kuni zinachochea moshi ambao una madhara kiafya, lakini vilevile ukataji wa miti unasababisha jangwa"***

***"Hii mitungi mliyopata mkaitumie vizuri na mkawe mabalozi wazuri kuhamasisha wengine wajikite na hii nishati safi ya kupikia ambayo hata Mhe. Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, amekuwa msitari wa mbele katika kuhakikisha watanzania wanatoka kwenye matumizi ya kuni hadi kwenye nishati safi ya kupikia"***, amesema Mhe. Santiel.


Kwa upande wake Mratibu wa zoezi hilo kutoka Doris Mollel Foundation, Bi. Dorice Laurent, ametoa shukrani kwa kampuni ya Oryx iliyosaidia kupatikana kwa mitungi 200 ambayo itasawadia wataalamu hao katika shughuli mbalimbali za mapishi.

Bi. Laurent ameongeza kuwa, lengo lao kama Foundation ni kuhakikisha wanaendelea kugawa mitungi hiyo nchi nzima ili kuokoa maisha ya Mama na Mtoto, ambao wanakuwa kwenye hatari kubwa ya kupatwa na changamoto ya kiafya, pindi wanapotumia nishati zisizo salama katika shughuli za mapishi.

Aidha, Muuguzi wa Mfawidhi katika Mkoa wa Shinyanga, Bi.Frola Kajumulla, amewashukuru Oryx Gas na Doris Mollel, kwa kugawa mitungi hiyo, akiamini itasaidia kuwa sehemu ya motisha kwa wengine, kutumia nishati safi ya kupikia.

Halikadhalika, Bi. Kajumulla ameishauri jamii kwa ujumla kuepukana na matumizi ya kuni ambayo kiafya si salama na kujikita kwenye nisharti safi ya kupikia ambayo ndiyo njia pekee itasaidia kutunza mazingira yanayomzunguka binadamu.

## MAKALA MAALUMU




Ini ni kiungo muhimu sana ndani ya miili yetu, hufanya kazi zaidi ya 500 ; moja ya kazi ni kuchuja na kuondoa sumu kutoka kwenye damu,kutokana na sababu mbalimbali kama pombe Iliyopita kiasi, sumu kwenye damu au maambukizi, Ini hupata shida na kuvimba na kushindwa kufanya kazi vizuri, hii hali huitwa homa ya Ini au Hepatitis.


Katika eneo la, Bara la Afrika maambukizi ya virusi vya homa ya Ini vipo vya vya aina 05 (A,B,C,D,E), aina mbili za Virusi (B na C) ndio sababu kuu za ugonjwa wa homa ya Ini na husambaa kupitia damu na Majimaji ya Mwili.

Homa ya Ini ni sawa na janga linaloua kimya kimya kulingana na takwimu za vifo kote dunia, Inakadiriwa kuwa kirusi cha homa ya Ini aina ya (B) pekee huua Watu takribani 600,000 kila mwaka kwa wastani zaidi ya Watu Bilioni mbili, yaani takribani asilimia 33 ya Watu wote ulimwenguni, wameambukizwa virusi vya HBV, na wengi wao hupona baada ya miezi michache alakini pia, Watu Milioni 350 hivi huendelea kuwa na Virusi hivyo mwilini, wengi huishi bila dalili na kuendelea kuambukiza watu wengine

## JINSI UNAVYOWEZA KUAMBUKIZWA VIRUSI VYA HOMA YA INI (B NA C)

Virusi vya homa ya Ini B Na C husambaa kupitia damu, Shahawa au maji maji mengine ya mwili,virusi hivi vina uwezo wa kusambaa na kuambukiza Mtu mara 100 zaidi ya virusi vya UKIMWI, njia hizi husambaza virusi hivi vya homa ya Ini;

1. Kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto
2. Mama aliye na maambukizi ya Hepatitis B kumuambukiza Mtoto Wakati wa kujifungua, iwapo hakutokuwa na juhudi za kitiba za kuzuia maambukizi kuna uwezekano hadi asilimia 90 kwa Mama Kumuambukiza Mtoto.
3.Kufanya Mapenzi na Mtu mwenye maambukizi ya virusi vya homa ya Ini
4. Kuchangia vifaa vyenye ncha kali kama sindano hasa kwa watumia dawa za kulevya au wachora tatoo na miswaki.
5.Kuongezewa damu ambayo inamaambukizi ya homa ya Ini.




## NANI YUPO KATIKA HATARI ZAIDI YA KUPATA MAAMBUKIZI YA HOMA YA INI

- Watoto Wachanga waliozaliwa na Mama aliye na maambukizi ya Virusi vya homa ya Ini
- Watu wanaofanya biashara Ya ngono
-Wanaume wanaofanya mapenzi na Wanaume wenzao
- Watu Wanaojidunga dawa za kulevya
- Mtu mwenye uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine ambaye anaishi na maambukizi ya Virusi vya homa ya Ini
- Wafanyakazi wa Sekta ya Afya
- Watu wa Familia wenye ndugu anayeishi na maambukizi ya kudumu ya Virusi vya homa ya Ini
- Wagonjwa wa Figo wanaotumia huduma za kusafisha damu (Dialysis)


>>> kutoka UK. NO 06

## DALILI ZA UGONJWA WA VIRUSI VYA HOMA YA INI

**DALILI ZA MUDA MFUPI (ACUTE HEPATITIS)**

1. Dalili hizi za Mwanzo hutokea ndani ya miezi 6 baada kuambukizwa Virusi vya homa ya Ini, hutokea kwa baadhi ya Watu hazitokei kwa kila Mtu.
2. Mgonjwa mwenye maambukizi ya virusi vya homa ya Ini hujiskia Kuumwa
3. Hupoteza hamu ya kula
4. Kichefuchefu na kutapika
5. Mwili kuuma mkojo kuwa na rangi iliyokolea kama Coca-Cola
6. Kupata manjano kwenye macho, viganja vya mikono/kucha au mwili mzima.

Aidha, kuna kundi Dogo la Wagonjwa wa homa ya Ini hupata ugonjwa mkali wa Ini na kusababisha Ini kushindwa kabisa kufanya kazi, pia huweza kusababisha kifo, hii hatua huitwa “Fulminant Liver Failure”.




## KWA NINI NI MUHIMU KUPIMA ILI KUJUA KAMA UNA MAAMBUKIZI

Watu wengi huishi na maambukizi ya virusi vya homa ya Ini bila kufahamu, kwa kawaida katika kipindi fulani cha maisha mtu mmoja kati ya watu watatu huambukizwa virusi vya homa ya Ini, baada ya kuambukizwa, kuna Kundi la Watu hubaki na maambukizi ya kudumu ya virusi vya homa ya Ini ambayo huwa hayana dalili yoyote na kuendelea Kuua Ini kimyakimya.

Dalili hizo huja kubainika baada ya miaka mingi kupita baada ya Mtu kuambukizwa na huonekana wakati tayari Ini limenyauka au lina kansa.

Hivyo, Mtu aliye na maambukizi ya kudumu ya virusi vya homa ya Ini aina B akianza matibabu mapema, anaweza kuzuia Ini lake lisiharibike sana. Pia kwa wenye maambukizi ya virusi aina C matibabu ya dawa kwa kipindi cha wiki 12 humaliza virusi vyote.

## CHANJO DHIDI YA VIRUSI VYA HOMA YA INI

Chanjo dhidi ya homa ya Ini hutolewa kwa watoto wote kama Ilivyo kwenye mpango wa Chanjo wa Taifa, pia hutolewa kwa watu wazima ambao hawajawahi kupata chanjo.
Chanjo hii hutolewa kwa njia ya Sindano, ambapo huwa ni sindano tatu 03 Sindano ya kwanza hutolewa baada ya kupimwa kujua kama hauna maambukizi, sindano ya pili hutolewa baada ya mwezi mmoja na sindano ya 03 baada ya miezi 06.

**MAKUNDI YAFUATAYO NI LAZIMA KUPATIWA CHANJO YA HOMA YA INI**

1. Watoto Wote
2. Watu wote wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI
3. Watu wote ndani ya Familia wanaoshi na ndugu aliyeambukizwa virusi vya homa ya Ini
4. Watu wote wanaotumia dawa za kufubaza kinga ya mwili (Immunosuppressive Therapy)
5. Watu wote wanaoufanya biashara ya ngono
6. Watu wote ambao wana mpenzi zaidi ya mmoja ndani ya miezi 6
7. Watu wenye maradhi ya kudumu ya Ini
8. Lakini pia Mtu Mwingine yeyote anahitaji kujikinga dhidi ya virusi vya homa ya Ini .

***MAKALA HII NI KWA HISANI YA TOVUTI YA HOSPITALI YA RUFAA YA LINDI- SOKOINE.***



# HABARI PICHA




Mgeni Rasmi wa Mahafali ya kwanza ya Chuo cha Uuguzi na Ukunga ST. Theresa na Bi. Agnes Mtawa (Katikati), akigonganisha glas na Mkuu wa Shirika la ST. Theresa ishara ya kuwatakia heri wahitimu.



Wahitimu wa Stashahada ya Uuguzi na Ukunga wa Chuo cha ST. Theresa Moshi Kilimanjaro, wakiwa katika maandamano ya kuelekea Kanisani kabla ya kuanza kwa Mahafali



Mgeni rasmi Msajili TNMC Bi. Agnes Mtawa, akiwa katika picha ya pamoja na Baba Askofu Ludovick Minde, Wahitimu na watawa mara baada ya Misa ya Shukrani iliyoongozwa na Baba Askofu Minde.




Mgeni rasmi Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa, akizindua Jarida la Chuo cha ST. Theresa, katika sherehe za Mahafali ya Kwanza ya Chuo hicho.




Afisa kutoka TNMC Bi. Rehema Msanjila (wa kwanza kulia) akiwahudumia wageni waliofika kutembelea Banda la TNMC katika Maonesho ya kimataifa ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es salaam.




Maafisa kutoka TNMC wakiwa katika Banda la Maonesho ya kitaifa ya Sabasaba yaliyofanyika Jijini Dar es salaam.

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA